*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1), 21-40*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.2

# Athari za Unyambulishaji katika Uelekezi wa Vitenzi vya Lugha ya Kimasai

*Anna Lomayani*[1] *na Perida Mgecha*[2]

## Ikisiri

Makala hii inachunguza namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi katika lugha ya Kimasai. Malengo mahususi ya makala hii ni kubainisha aina za uelekezi, kueleza uelekezi unavyojitokeza na kuchambua namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi katika lugha ya Kimasai. Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Uhusika iliyoasisiwa na Noam Chomsky (1981). Watoataarifa wamepatikana kwa mbinu za usampulishaji tajiriba na tajwa. Data za makala hii zimekusanywa kwa mbinu za tafsiri na ukalimani na uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia mbinu ya kusimba maudhui. Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa lugha ya Kimasai ina aina tatu za uelekezi ambazo ni uelekezi wa yambwa moja, wa yambwa mbili na wa yambwa kapa. Aidha, utafiti umebaini kuwa katika lugha ya Kimasai, yambwa hujitokeza baada ya mtenda ambayo ni tofauti na lugha nyingine, kama vile Kiswahili ambapo yambwa hutokea baada ya kitenzi. Kwa upande wa athari za unyambulishaji katika uelekezi wa vitenzi vya lugha ya Kimasai, husababisha kuongezeka, kuhamishwa au kudondoshwa kwa yambwa. Hata hivyo, tafiti zaidi zinazochunguza vipengele vingine vya kiisimu katika lugha ya Kimasai zinahitajika.

## 1.0 Utangulizi

Tafiti mbalimbali zimeonesha kuwa lugha nyingi zina uelekezi. Hata hivyo, utokeaji wa uelekezi huo huweza kutofautiana kati ya lugha moja na nyingine kutokana na mgawanyo wa lugha husika ambao umezingatia sifa mbalimbali zikiwamo za kisarufi (kama vile, matamshi, maumbo, muundo na maana). Mathalani, nchini Tanzania, lugha zimegawanywa katika makundi makuu manne.

[1] Mhitimu wa Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Tanzania. Baruapepe: lomayanianna@gmail.com

[2] Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Tanzania. Baruapepe: peridamgecha@gmail.com

Kundi la kwanza ni jamiilugha za Kibantu ambapo lugha nyingi zinaingia hapa, kama vile Kimeru, Kihaya, Kipare, Kisukuma, Kigogo, Kizigua na Kibena. Kundi jingine ni jamiilugha ya Kushitiki ambapo Kiiraki, Kiburunge na Kigorowa vinahusika. Kundi jingine ni la jamiilugha za Khoisani ambazo ni Kisandawe, Kihatsa, Kindega, Kitindiga na Kihadzapi. Kundi la mwisho ni Nailotiki ambalo lugha ya Kimasai inahusika (Rugemalira, 2005; Nurse na Heine, 2008).

Kuna tafiti na maandiko mbalimbali yanayochambua dhana ya uelekezi. Mathalani, Haji (2018) katika utafiti wa lahaja ya Kitumbatu amechambua uelekezi katika kirai kitenzi na kudhihirisha kuwa kirai kitenzi hicho huweza kubeba nomino moja au mbili. Haji) anaeleza kuwa kitenzi elekezi ni kitenzi ambacho kutokana na maana pamoja na umbile lake kinahitaji kukamilishwa na nomino. Kitenzi kinachofuatwa na nomino mbili kinajulikana kama kitenzi cha yambwa mbili au kitenzi chenye uelekezi mara dufu. Katika uchambuzi wake, amebainisha miundo tofauti ya virai vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu pamoja na vitenzi elekezi na visivyoelekezi vya lahaja hiyo. Hata hivyo, utafiti wa Haji (keshatajwa) umejikita katika Kitumbatu ambacho ni moja ya lugha za Kibantu. Muundo wa tungo za Kitumbatu ni tofauti na muundo wa tungo za Kimasai, hivyo, muundo huu pia unaathiri utokeaji wa uelekezi baina ya lugha hizi mbili.

Gitonga (2014) amechunguza upatanishi wa kisarufi hasa uliopo baina ya virai nomino na virai vitenzi katika lahaja ya Kichuka. Katika utafiti wake, Gitonga anaonesha kategoria miundo ambazo ni nomino, kivumishi, kiwakilishi na kitenzi. Katika vitenzi, ameonesha kuwa Kichuka huwa na kitenzi kielekezi na kisoelekezi, dhana ambayo hupatikana kabla na baada ya mnyambuliko. Utafiti wa Gitonga (2014) unafaa kwenye makala hii kwani umegusia suala la vitenzi elekezi na sielekezi kwa kuonesha upatanisho wa kisarufi wa mofu ya yambwa tendwa na tendewa zinazobebwa katika kitenzi. Hata hivyo, utafiti wa Gitonga umefanyika katika lahaja ya Kichuga wakati utafiti huu umefanyika katika lugha ya Kimasai. Miundo ya tungo za Kinailotiki ni tofauti na ile ya lugha za Kibantu. Pia, makala hii imeangalia athari za unyambulishaji katika uelekezi na sio upatanisho wa kisarufi. Pamoja na hayo, wapo waliotafiti kuhusu uelekezi wakihusisha na dhana ya unyambulishaji wa vitenzi. Gituru (2019) amehusisha dhana ya uelekezi na unyambulishaji wa vitenzi katika kauli ya kutendea. Amebaini kuwa vitenzi elekezi na sielekezi huathiriwa na unyambulishaji katika Kigĩchũgũ na hivyo kuleta athari kisintaksia. Utafiti huu umefaa katika makala hii katika kuchambua namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi vya lugha ya Kimasai ambayo ni Kinailotiki. Hata hivyo, Gituru (keshatajwa) amegusia uelekezi katika kauli ya kutendea ilihali makala hii imechambua namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi katika kauli saba zinazopatikana katika lugha ya Kimasai.

Nchimbi (2020) amechambua utokeaji wa yambwa na dhima zake katika lugha za Kimatengo na Kiswahili. Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba sifa ya kiwango cha uelekezi wa maumbo asili ya vitenzi ndiyo huamua hali ya kitenzi kuwa na yambwa kapa, yambwa moja au yambwa mbili. Pamoja na utafiti huu kuongeza maarifa ya makala hii katika kubaini aina za yambwa na utokeaji wake,

bado kuna haja ya kuchunguza zaidi katika lugha ya Kimasai. Hii ni kwa sababu, muundo wa tungo za Kimatengo ni tofauti na ule wa tungo za Kimasai. Aidha, Charwi (2017) amechanganua unyambulishaji wa vitenzi ili kuonesha uelekezi unavyojitokeza katika lugha ya Kikuria na lugha nyingine za Kibantu, kama vile Kinyambo, Kinyamwezi na Kibosho. Amebaini kuwa mofu za kauli ya utendea na usababishi huathiri si tu kitenzi si elekezi kuwa elekezi bali pia kitenzi elekezi kuhitaji kipashio kingine ili kukamilisha maana iliyokusudiwa. Pia, imebainika kuwa kauli za utendano, utendwa na utendeka hukiondolea kitenzi uwezo wa kuhitaji yambwa. Hivyo, huleta mabadiliko ya kidhima baina ya vipashio vya sentensi. Hata hivyo, utafiti wa Charwi (2017) umejikita katika lugha za Kibantu ambazo utokeaji wa yambwa ni tofauti na ule uliopo katika tungo za Kimasai.

Asiimwe (2011) amechunguza unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Runyankole. Amebainisha kuwa unyambulishaji wa vitenzi katika Runyankole unahusisha mizizi ya vitenzi ambapo mofimu nyambulishi hupachikwa. Anaonesha kuwa mofimu nyambulishi za usababishi huanza kwanza katika kitenzi kabla ya utendwa. Hata hivyo, utafiti wa Asiimwe umejikita katika kuchambua mofu za unyambulishaji katika vitenzi bila kuhusisha namna unyambulishaji huo unavyoathiri uelekezi wa vitenzi hivyo. Hivyo, makala hii imechambua namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi katika lugha ya Kimasai.

Khamis (2008) amechambua kitenzi cha Kiswahili kwa kuchunguza athari ya viambishi nyambulishi juu ya mizizi na mashina. Amebainisha kuwa unyambulishaji wa vitenzi ni mfumo wa sheria za kuunda maneno ambao kazi yake ni kuunda maneno mapya. Uundaji wa maneno hayo hufanywa kwa utaratibu wa kuongeza, kupunguza, au kufasili upya dhima zilizomo ndani ya sulubu dhima ya kitenzi tu. Mathalani, anaeleza kuwa sentensi tenda na tendwa zinahusianishwa na sheria ya ufasiri upya wa dhima, sentensi elekezi na zisizoelekezi zinahusianishwa na sheria za unyambulishaji ongezi na punguzi dhima kufuatana na aina ya unyambulishi. Sentensi tendeka zinahusianishwa na sheria za upunguzaji dhima; hii ni pamoja na tofauti za kimofolojia na fasili za kisemantiki. Sentensi fanyizi na zisizofanyizi zinahusianishwa na sheria ya uongezaji dhima. Hata hivyo, Khamis (2008) amejikita zaidi katika suala la unyambulishaji na athari ya vinyambuo hivyo katika lugha ya Kiswahili ambayo miundo ya tungo zake ni tofauti na Kimasai. Makala hii pamoja na kuangalia athari za unyambulishaji, pia imechambua namna uelekezi unavyojitokeza katika sentensi za lugha ya Kimasai.

Ingawa tafiti mbalimbali kama vile Charwi (2017), Gituru (2019) na Nchimbi (2020) zimefanyika kuhusu uelekezi, nyingi zimejikita katika lugha za Kibantu. Makala hii imechunguza namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi katika lugha ya Kimasai, ambayo ni familia ya Kinailotiki. Muundo wa sentensi za lugha za Kibantu ni tofauti na wa sentensi za lugha ya Kimasai. Sentensi ya lugha ya Kimasai huanza na kitenzi halafu hufuatiwa na mtenda ambaye hufuatiwa na yambwa, wakati lugha nyingi zilizofanyiwa tafiti kuhusu uelekezi hasa za Kibantu muundo wake huanza na mtenda; na baada ya mtenda hufuata kitenzi kisha kufuatiwa na yambwa. Mpangilio huu una athari pia katika

suala la uelekezi wa vitenzi. Hivyo, imeonekana kuna haja ya kuchunguza uelekezi katika lugha ya Kimasai ili kuona namna unavyojitokeza katika tungo zenye mpangilio huo na kuchambua athari ya unyambulishaji katika uelekezi wa vitenzi vya lugha ya Kimasai. Kwa kufanya hivyo, makala hii inaongeza maarifa miongoni mwa wanaisimu hasa isimu-linganishi katika kulinganisha uelekezi katika lugha za Kibantu na za Kinailotiki ambapo mpangilio wa tungo zake ni tofauti.

## 2.0 Nadharia Iliyotumika

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Uhusika iliyoasisiwa na Noam Chomsky (1981). Nadharia ya Uhusika huelekeza ugavi wa virai nomino vinavyobainika kifonetiki kwa kuvihusisha na dhima dhahania. Idadi ya uhusika dhima hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa ujumla, dhima zinazohusishwa ni:

i. Uhusika kiima ambao ni umbo la uhusika unaowekwa kwenye nomimo au kiwakilishi chake kuonesha kuwa nomino au kiwakilishi hicho ni kiima;
ii. Uhusika yambwa unaoonesha nomino katika tungo inayotendewa au inayotendwa;
iii. Uhusika tendea huonesha yule anayeathirika na jambo linalotendwa; na
iv. Uhusika milikishi huonesha kitu kinachomilikiwa.

Misingi ya nadharia hii imetumika katika kuongoza uchambuzi wa data za makala hii. Msingi wa uhusika yambwa unaoonesha nomino katika tungo inayotendewa au inayotendwa umesaidia kuonesha ni aina zipi za uelekezi zinajitokeza katika lugha ya Kimasai. Katika hali hii, aina ya uelekezi yenye kitenzi kilichobeba yambwa ni kitenzi elekezi na kitenzi ambacho hakijabeba yambwa si elekezi. Pia, msingi huu umetumika katika kuchambua utokeaji wa yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi zilizo na uelekezi. Msingi wa uhusika tendea pamoja na wa uhusika yambwa katika kuonesha nomino inayotendewa au inayotendwa katika tungo imesaidia katika kuchambua namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi katika lugha ya Kimasai (Noam Chomsky, 1981).

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti unaohusu athari za unyambulishaji katika uelekezi wa vitenzi vya lugha ya Kimasai ni wa kitaamuli. Mbinu za usampulishaji zilizotumika ni usampulishaji tajiriba na tajwa. Mbinu ya usampulishaji tajiriba imetumika kuwachagua watoataarifa kumi ambao ni Wamasai wenye umri kuanzia miaka 50 na kuendelea. Sababu za kuteua umri huu ni kwamba hawa ni watu ambao wana tajiriba na uzoefu mkubwa wa maisha ikiwamo kuwa na uelewa kuhusu lugha ya Kimasai. Mbinu hii pia imezingatia kigezo cha watoataarifa wanaojua kusoma na kuandika kutoka katika kata mbili. Hii ni kwa sababu walipaswa kutafsiri sentensi kutoka lugha ya Kiswahili kwenda katika Kimasai. Pamoja na mbinu ya usampulishaji tajiriba kutumika, usampulishaji tajwa umetumika katika kuwabainisha

watoataarifa saba ambao walikuwa na sifa ya kutokuhama kwenda kuishi na jamiilugha nyingine. Hivyo, mbinu hii ilitumika kuwapata watoataarifa saba ambapo watatu wanatoka katika Kata ya Oldonyosambu na wanne kutoka Kata ya Oldonyowass. Watoataarifa hawa ndio waliotumiwa kukalimani sentensi 95 kutoka lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kimasai.

Usampulishaji tajwa pia ni mbinu iliyotumiwa na watafiti. Kwayo, walimwomba mtoataarifa wa kwanza awaelekeze kwa mtu mwingine ambaye alifaa katika kutoa taarifa. Hivyo, mtoataarifa wa kwanza aliyepatikana kutokana na uzoefu na tajiriba aliyokuwa nayo alitumika kuwapata watoataarifa wengine. Mbinu hii ya kutajana ilitumika mpaka utoshelevu wa taarifa husika ulipokamilika. Kwa ujumla, sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni watoataarifa 17, yaani 8 kutoka katika Kata ya Oldonyosambu na 9 kutoka Kata ya Oldonyowass.

Data ya utafiti huu imekusanywa kwa mbinu za tafsiri na ukalimani. Watafiti walitunga sentensi 95 za Kiswahili kwa kuzingaatia usanifu wa lugha husika. Sentensi hizo zilikuwa na vitenzi vilivyonyambuliwa katika kauli mbalimbali, na zenye uelekezi na zisizo na uelekezi kulingana na malengo mahususi ya utafiti. Watoataarifa kumi walipewa sentensi hizo 95 kila mmoja ili wazitafsiri kutoka lugha ya Kiswahili kwenda katika Kimasai. Wote walipewa sentensi za aina moja, zilizokuwa zimeundwa na vitenzi vilivyonyambuliwa katika kauli mbalimbali, zenye uelekezi na zisizo na uelekezi ndani yake. Katika mbinu ya ukalimani, watoataarifa saba waliombwa kushiriki kutoa taarifa kwa kutajiwa sentensi mojamoja iliyopo katika lugha ya Kiswahili na kuwataka wakalimani sentensi hizo kwa lugha ya Kimasai. Sentensi zilezile 95 zilizotumika katika tafsiri ndizo zilizotumika pia katika mbinu hii ya ukalimani. Data zilizopatikana kwa mbinu ya ukalimani zimerekodiwa kwa njia ya simu. Hivyo, watafiti wametumia mbinu za tafsiri na ukalimani ili kuweza kupata sentensi za Kimasai ambazo ziliwawezesha kubainisha aina za uelekezi, kueleza namna uelekezi unavyojitokeza pamoja na kuchambua namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi katika lugha ya Kimasai. Data zilizopatikana, zilichanganuliwa kwa mbinu ya kusimba maudhui.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti na Mjadala

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa lugha ya Kimasai ina aina tatu za uelekezi ambazo ni uelekezi wa yambwa moja, wa yambwa mbili na wa yambwa kapa. Aidha, utafiti umebaini kuwa katika lugha ya Kimasai, yambwa hujitokeza baada ya mtenda. Katika uelekezi wa yambwa moja mtendwa hutokea mara tu baada ya mtenda wakati katika uelekezi wa yambwa mbili mtendewa hutokea mara baada ya mtenda na mtendwa hutokea mara tu baada ya mtendewa. Kwa upande wa athari za unyambulishaji katika uelekezi wa vitenzi vya lugha ya Kimasai, husababisha kuongezeka, kuhamishwa au kudondoshwa kwa yambwa. Matokeo haya yamechambuliwa na kujadiliwa kama ifuatavyo:

### 4.1 Aina za Uelekezi na Ujitokezaji wake katika Kimasai

Aina tatu za uelekezi zilizobainishwa na makala hii zimewasilishwa na kuchambuliwa kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Uelekezi wa Yambwa Moja

Uelekezi wa yambwa moja ni aina ya uelekezi wenye uwezo wa kubeba yambwa moja tu. Yambwa hiyo huwa ni tendwa. Katika uelekezi wa yambwa moja, yambwa tendwa hutokea mara tu baada ya mtenda. Rejea Data Na. 1:

**Data Na. 1:**

| | | |
|---|---|---|
| i. | **Kimasai:** | *Ebuing'a **olapuroni**.* |
| | **Kiswahili:** | Amemkamata **mwizi**. |
| ii. | **Kimasai:** | *Etudung'o engerai **olkimojino**.* |
| | **Tafsiri sisisi:** | Amejikata mtoto **kidole**. |
| | **Kiswahili:** | Mtoto amejikata **kidole**. |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Vitenzi vilivyomo katika Data Na. 1 vinahitaji yambwa moja ili kujikamilisha kimawasiliano. Maneno yaliyokozwa wino ni yambwa tendwa ambazo zimetokana na vitenzi elekezi vya yambwa moja. Kitenzi elekezi huhitaji yambwa katika kukidhi dhima za dhamira mbalimbali kulingana na uhitaji wake. Katika Data Na. 1, yambwa imetokea mara tu baada ya mtenda. Hivyo, kimeanza kitenzi halafu akafuata mtenda kisha kufuatiwa na yambwa tendwa.

#### 4.1.2 Uelekezi wa Yambwa Mbili

Uelekezi wa yambwa mbili ni aina ya uelekezi ambao unahitaji kujalizwa kwa yambwa mbili ili uweze kujikamilisha kisarufi. Vitenzi elekezi vya yambwa mbili vinajitokeza katika lugha ya Kimasai kama inavyofafanuliwa katika Data Na. 2.

**Data Na. 2:**

| | | |
|---|---|---|
| i. | **Kimasai:** | *Etuudo olramatani **olndamoyai oltidu.*** |
| | **Tafsiri sisisi:** | Amemchoma daktari **mgonjwa sindano.** |
| | **Kiswahili:** | Daktari amemchoma **mgonjwa sindano.** |
| ii. | **Kimasai:** | *Etoorutwo ilapurok **engerai ingoshola**.* |
| | **Tafsiri sisisi:** | Wamemnyang'anya majambazi **mtoto fedha.** |
| | **Kiswahili:** | Majambazi wamemnyang'anya **mtoto fedha.** |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 2, maneno yaliyokolezwa wino ni yambwa mbili ambazo ni yambwa tendwa na yambwa tendewa. Hivyo, vitenzi '*etuudo'* (amemchoma) na '*etoorutwo*' (wamemnyang'anya) ni vitenzi elekezi vya yambwa mbili ambapo '*olndamoyai*' (mgonjwa) na '*engerai*' (mtoto) ni yambwa tendewa na '*oltidu*'

(sindano), na ‘*ingoshola*’(fedha) ni yambwa tendwa. Hivyo, katika lugha ya Kimasai, yambwa tendewa hujitokeza mara tu baada ya mtenda na yambwa tendwa hujitokeza mara tu baada ya mtendewa kama Data Na. 2 inavyoonesha.

**4.1.3 Uelekezi wa Yambwa Kapa**

Uelekezi wa yambwa kapa huhusisha vitenzi ambavyo haviwezi kubeba yambwa. Mifano ya uelekezi wa yambwa kapa katika lugha ya Kimasai ni kama ifuatavyo katika Data Na. 3.

**Data Na. 3:**

| | | |
|---|---|---|
| i. | **Kimasai:** | *Eishirita engerai.* |
| | **Tafsiri sisisi:** | Analia mtoto. |
| | **Kiswahili:** | Mtoto analia. |
| ii. | **Kimasai:** | *Etwa engine.* |
| | **Tafsiri sisisi:** | Amekufa mbuzi. |
| | **Kiswahili:** | Mbuzi amekufa. |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Data Na. 3 inaonesha kuwa vitenzi hivyo sio elekezi. Hivi ni aina ya vitenzi ambavyo havihitaji kujalizwa na yambwa ili kukamilisha maana katika sentensi. Kwa ujumla, aina za uelekezi zinazojitokeza katika lugha ya Kimasai ni uelekezi wa yambwa moja, wa yambwa mbili pamoja na wa yambwa kapa. Katika uelekezi wa yambwa moja, nomino yambwa hutokea mara tu baada ya mtenda wakati katika uelekezi wa yambwa mbili, mtendewa hutokea mara baada ya mtenda, na mtendwa hutokea mara tu baada ya mtendewa. Hata hivyo, uelekezi kapa hauna utokeaji wa yambwa kwa kuwa vitenzi vyake havihitaji yambwa ili kukamilisha taarifa. Matokeo haya yanashadidiwa na msingi wa kwanza wa Nadharia ya Uhusika uliojikita katika uhusika yambwa. Msingi huu unaonesha kuwa kitenzi katika tungo kinaweza kubeba yambwa tendwa peke yake au kikabeba yambwa tendewa na yambwa tendwa kwa pamoja.

Kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu, katika lugha ya Kimasai kuna vitenzi vinavyohitaji yambwa na vingine visivyohitaji yambwa. Uelekezi wa yambwa moja huhitaji yambwa moja na uelekezi wa yambwa mbili huhitaji yambwa mbili, yaani mtendwa na mtendewa. Sifa hii inajidhihirisha pia katika lugha ya Kikuria ambapo Charwi (2017) anaonesha kuwa vitenzi si-elekezi havihitaji yambwa wakati vitenzi elekezi huhitaji yambwa moja au mbili kulingana na sifa ya uelekezi ya kitenzi chenyewe. Aidha, katika lugha ya Kimasai uelekezi kapa hauhitaji yambwa katika kukamilisha taarifa. Hata hivyo, vitenzi hivi hufuatiwa na vielezi au virai vielezi (Oichoe, 2005). Vilevile, Chisia (2012) ameonesha kuwa katika lugha ya Kiswahili baadhi ya vitenzi hueleweka bila kuongeza yambwa kwani kuongeza huko hufanya sentensi kukosa mantiki.

Kwa upande wa utokeaji wa uelekezi katika lugha ya Kimasai, vitenzi elekezi vya yambwa moja, yambwa hujitokeza mara tu baada ya mtenda. Hivyo, muundo wake ni:

**Kitenzi + mtenda + yambwa tendwa**

Hii imekuwa tofauti na lugha nyingi za Kibantu kama vile Kigĩchũgũ (Gituru, 2019) na Kimatengo (Nchimbi, 2020) ambapo nomino ya yambwa katika uelekezi wa yambwa moja hutokea mara baada ya kitenzi. Vilevile, uelekezi wa yambwa mbili unaonesha kuwa yambwa zote mbili hutokea mara baada ya mtenda ambapo yambwa tendewa hutokea baada ya mtenda, halafu yambwa tendwa hutokea mara tu baada ya yambwa tendewa. Hivyo muundo wake ni:

**Kitenzi + Mtenda +Yambwa tendewa + Yambwa tendwa**

Hivyo, utokeaji wa uelekezi wa yambwa mbili katika lugha ya Kimasai ni tofauti na lugha za Kibantu. Kwa mfano, katika lugha ya Kiswahili yambwa hutokea mara baada ya kitenzi ambapo hufuata yambwa tendewa na yambwa tendwa kama ilivyofupishwa:

**Mtenda + Kitenzi + Yambwa tendewa + Yambwa tendwa**

Uelekezi kapa hauna utokeaji wa yambwa kwa kuwa kitenzi hakihitaji yambwa ili kukamilisha taarifa. Vitenzi visoelekezi vinapowekewa yambwa vinasababisha urudiaji wa taarifa usiokuwa wa lazima. Hivyo, imebainika kuwa katika lugha ya Kimasai vitenzi si elekezi vinaeleweka bila ya kuwa na yambwa katika sentensi.

### 4.2 Athari za Unyambulishaji katika Uelekezi wa Vitenzi vya Kimasai

Makala hii imeonesha namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi kwa kutumia kauli saba za unyambulishaji ambazo ni kauli ya utendea, utendana, utendeana, utendwa, utendewa, utendeka na kauli ya utendesha. Data zimewasilishwa kwa kuzingatia michakato inayohusika katika vitenzi elekezi vya yambwa moja, vya yambwa mbili na vya yambwa kapa.

#### 4.2.1 Athari ya Utendea katika Uelekezi wa Vitenzi vya Kimasai

Mofu za kauli ya utendea huathiri uelekezi zinapopachikwa kwenye kitenzi kilichopo katika kauli ya utenda. Kauli ya utendea ni kitendo cha kufanya kitendo kwa ajili ya mtu mwingine. Mofu ya kauli ya utendea katika lugha ya Kimasai ni ***-aki*** na ***-oki***. Hali hii inadhihirika katika Kimasai kama ifuatavyo: katika uelekezi wa yambwa moja, kauli ya utendea husababisha kuongezeka kwa yambwa moja. Hii inadhihirika katika Data Na. 4:

**Data Na. 4:**

Kauli ya utenda

**Kimasai:** *Eisujita enganashe **emalaga**.*

**Tafsiri sisisi:** Anaosha dada **kijiko**

**Kiswahili:** Dada anaosha **kijiko**.

Kauli ya utendea
**Kimasai:** *Eisuj-**aki**-ta enganashe **engerai emalaga.***
**Tafsiri sisisi:** Anamwoshea dada **mtoto kijiko**.
**Kiswahili:** Dada anamwoshea **mtoto kijiko**.
**Chanzo:** Uwandani (2022)

Athari inayowasilishwa katika Data Na. 4 ni kuongezeka kwa yambwa moja. Kitenzi kinapokuwa kwenye kauli ya utenda kinakuwa ni kitenzi elekezi cha yambwa moja ambacho baada ya kupachikwa mofu ya kauli ya utendea kimekuwa kitenzi elekezi cha yambwa mbili. Hivyo, katika kauli ya utenda kitenzi chenye yambwa tendwa, baada ya kupachika mofu ya utendea ***-aki-*** yambwa tendewa imeongezeka.

Katika uelekezi wa yambwa mbili, kauli ya utendea haisababishi athari yoyote. Hii inadhihirika katika Data Na. 5:

**Data Na. 5:**
Kauli ya utendea
**Kimasai:** *Inas-**aki-ta** papa **engerai oloongukuuni.***
**Tafsiri sisisi:** *Anamsimulilia baba **mtoto hadithi**.
**Kiswahili:** Baba anamsimulia **mtoto hadithi**.
**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 5 hakuna athari yoyote ya kimuundo, hivyo, kitenzi elekezi cha yambwa mbili kinabaki kuwa na yambwa mbili hata baada ya kupachikwa mofu ya utendea ***-aki***. Kwa upande mwingine, mofu ya kauli ya utendea inapopachikwa kwenye kitenzi chenye uelekezi wa yambwa kapa husababisha kuzaa yambwa moja. Hii inadhihirika katika Data Na. 6:

**Data Na. 6:**
Kauli ya utenda
**Kimasai:** *Eishirita engerai.*
**Tafsiri sisisi:** Analia mtoto.
**Kiswahili:** Mtoto analia.

Kauli ya utendea
**Kimasai:** *Eishir-**aki**-ta engerai **endaa.***
**Tafsiri sisisi:** Analilia mtoto **chakula**.
**Kiswahili:** Mtoto analilia **chakula**.
**Chanzo:** Uwandani (2022)

Athari inayowasilishwa katika Data Na. 6 ni kutokea kwa yambwa moja ambapo kitenzi chenye kauli ya utenda kilikuwa ni kitenzi si elekezi, lakini baada ya kupachika mofu ***-aki-*** ya kauli ya utendea imesababisha kuzaa yambwa moja;

hivyo, kitenzi kubadilika sifa yake kutoka kitenzi si-elekezi na kuwa kitenzi elekezi cha yambwa moja ambapo ‘*endaa*’ (chakula) ni yambwa tendwa.

**4.2.2 Athari za Utendana katika Uelekezi wa Vitenzi vya Kimasai**

Kauli ya utendana ni hali inayorejelea tendo lifanywalo na kiima kuwa ndilo huweza pia kufanywa na yambwa. Kimofolojia mofu ya utendana huhusisha pande mbili katika utendaji wa kiwango sawa. Data za utafiti zinabainisha kuwa mofu za kauli ya utendana katika Kimasai ni ***ate*** na **-*ote***. Mofu hizi ndizo zinazoonesha kuwa kila mhusika katika kiima hutenda tendo lilelile kwa mwenzie. Athari za kauli ya utendana katika uelekezi hutokea katika lugha ya Kimasai katika ngazi tatu za uelekezi ambazo ni uelekezi wa yambwa moja, uelekezi wa yambwa mbili na uelekezi wa yambwa kapa.

Katika lugha ya Kimasai, data za utafiti zinabainisha kuwa kauli ya utendana huleta athari katika uelekezi wa yambwa moja. Athari hiyo ni kuhamishwa kwa yambwa na kwenda kukaa katika nafasi ya mtenda. Hii inadhihirika katika Data Na. 7:

**Data Na. 7:**

Kauli ya utenda

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Iyemihe **Lomayani Ana**.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Ameoa **Lomayani Ana**. |
| **Kiswahili:** | Lomayani amemwoa **Ana**. |

Kauli ya utendana

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Iyemihe-**ote** Lomayani oo Ana.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Wameoana Lomayani na Ana. |
| **Kiswahili:** | Lomayani na Ana wameoana. |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 7, kitenzi katika kauli ya utenda ni kitenzi elekezi cha yambwa moja ambapo baada ya kupachika kauli ya utendana imesababisha kuhamishwa kwa yambwa kwenda kukaa sehemu ya mtenda. Hivyo, kitenzi kuwa si-elekezi ambapo yambwa ‘Ana’ imepata sifa ya kuwa mtenda. Pia, data zinadhihirisha kuwa kupachika kauli ya utendana katika kitenzi chenye uelekezi wa yambwa mbili huleta athari katika sentensi. Athari inayojitokeza ni kuhamishwa kwa yambwa na kwenda kukaa sehemu ya mtenda kama inavyodhihirika katika Data Na. 8:

**Data Na. 8:**

Kauli ya utenda

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Inasa eletia **ingerai oloongukuuni**.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Wanawasimulia wanakijiji **watoto hadithi**. |
| **Kiswahili:** | Wanakijiji wanawasimulia **watoto hadithi**. |

Kauli ya utendana

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Inasakin-**ote** elatia oo ingerai **oloongukuuni**.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Wanasimuliana wanakijiji na watoto **hadithi**. |
| **Kiswahili:** | Wanakijiji na watoto wanasimuliana **hadithi**. |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 8, athari inayotokea baada ya kupachikwa mofu ya kauli ya utendana kwenye kitenzi chenye uelekezi wa yambwa mbili ni kuhamishwa kwa yambwa kwenda kukaa sehemu ya mtenda, ambapo yambwa '*ingerai*' (watoto) imechukua nafasi ya mtenda katika sentensi yenye kauli ya utendana. Hivyo, kupachika mofu ya kauli ya utendana kumesababisha sentensi kuhitaji yambwa moja tu, kutoka kitenzi elekezi cha yambwa mbili na kuwa kitenzi elekezi cha yambwa moja. Hata hivyo, imebainika kuwa kauli ya utendana haina athari yoyote katika uelekezi wa yambwa kapa kwa sababu vitenzi si-elekezi havibebi yambwa kwa asili yake. Ili kitenzi kipelekwe katika kauli ya utendana ni lazima kiwe na yambwa.

### 4.2.3 Athari za Utendeana katika Uelekezi wa Vitenzi vya Kimasai

Kauli ya utendeana husababisha yambwa kuhamia kwenye nafasi ya mtenda. Katika lugha ya Kimasai, mofu ya kauli ya utendeana ni ***-akin-*** na ***okin-***. Kauli ya utendeana hujumuisha kauli mbili ambazo ni kauli ya utendea na kauli ya utendana. Katika lugha ya Kimasai, kauli ya utendeana haina athari katika uelekezi wa yambwa moja. Data za utafiti zinadhihirisha katika Data Na. 9:

**Data Na. 9:**

Kauli ya utenda

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Eibookito Nabikieki oo Namayani **indare**.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Anachunga Nabikieki na Namayani **mbuzi**. |
| **Kiswahili:** | Nabikieki na Namayani wanachunga **mbuzi**. |

Kauli ya utendeana

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Eibo-**okin**-o Nabikieki oo Namayani **indare**.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Wanachungiana Nabikieki na Namayani **mbuzi**. |
| **Kiswahili:** | Nabikieki na Namayani wanachungiana **mbuzi**. |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 9, inabainika kuwa kauli ya utendeana haina athari yoyote katika uelekezi wa yambwa moja. Hivyo, kitenzi elekezi cha yambwa moja kimebaki kuwa kitenzi elekezi cha yambwa moja katika lugha ya Kimasai.

Katika lugha ya Kimasai, imebainika kuwa kauli ya utendeana huleta athari kwa kupunguza yambwa moja ambayo ni yambwa tendewa katika sentensi, na yambwa hii kuhamia sehemu ya mtenda. Hii inadhihirika katika Data Na. 10:

**Data Na. 10:**

Kauli ya utenda
**Kimasai:** *Eyerakita elatia **ingera endaa***
**Tafsiri sisisi:** Wanawapikia wanakijiji **watoto chakula**.
**Kiswahili:** Wanakijiji wanawapikia **watoto chakula**.

Kauli ya utendeana
**Kimasai:** *Eyer-**akin**-o elatia oo ingerai **endaa**.*
**Tafsiri sisisi:** Wanapikiana wanakijiji na watoto **chakula**.
**Kiswahili:** Wanakijiji na watoto wanapikiana **chakula**.

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 10, mofu ***-akin-*** ya kauli ya utendeana imesababisha yambwa tendewa '*ingera*' (watoto) kuwa sehemu ya mtenda. Hivyo, kitenzi chenye uelekezi wa yambwa mbili katika kauli ya utenda, baada ya kupachikwa kauli ya utendeana kimekuwa kitenzi cha uelekezi wa yambwa moja. Hata hivyo, data za watoataarifa zinabainisha kuwa kauli ya utendeana haina athari katika uelekezi kapa; hivyo kitenzi si elekezi kinabaki kuwa si elekezi. Hii ni kwa sababu, kauli ya utendeana huhusisha mageuzi ya kisintaksia ambayo ni kuhamishwa kwa kipashio yambwa na kukipa hadhi ya mtenda. Kanuni hii haifanyi kazi katika vitenzi si elekezi.

### 4.2.4 Athari za Utendwa katika Uelekezi wa Vitenzi vya Kimasai

Kauli ya utendwa husababisha yambwa kuchukua nafasi ya mtenda. Hii ina maana kuwa tendo linampata mtu au kitu bila yeye kukitenda kitendo hicho. Katika lugha ya Kimasai, mofu ya kauli ya utendwa ni ***-i, -aki*** na ***-oki***.

Katika uelekezi wa yambwa moja, kauli ya utendwa husababisha yambwa tendwa kuchukua nafasi ya mtenda. Hii inadhihirika katika Data Na.11:

**Data Na. 11:**

Kauli ya utenda
**Kimasai:** *Enyor yeyo **engerai**.*
**Tafsiri sisisi:** Anampenda mama **mtoto**.
**Kiswahili:** Mama anampenda **mtoto**.

Kauli ya utendwa
**Kimasai:** *Etonyorr-**i** engerai oo yeyo.*
**Tafsiri sisisi:** Anapendwa mtoto na mama.
**Kiswahili:** Mtoto anapendwa na mama.

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 11 kauli ya utendwa imesababisha yambwa kuchukua nafasi ya mtenda. Hivyo, kitenzi elekezi mara moja kimekuwa si elekezi baada ya kupachikwa kauli ya utendwa.

Kauli ya utendwa pia husababisha yambwa tendewa kuhamishiwa kwenye nafasi ya mtenda katika uelekezi wa yambwa mbili. Hii inadhihirika katika Data Na. 12:

**Data Na. 12:**

Kauli ya utenda
**Kimasai:** *Etoshooko ilaitengenok **olaiteng'enani oldoo.***
**Tafsiri sisisi:** Amempigia mwanafunzi **mwalimu kelele**.
**Kiswahili:** Mwanafunzi amempigia **mwalimu kelele**.

Kauli ya utendwa
**Kimasai:** *Etosho-**oki** olaiteng'enani **oldoo** oo ilaitengenok.*
**Tafsiri sisisi:** Amepigiwa mwalimu **kelele** na mwanafunzi.
**Kiswahili:** Mwalimu amepigiwa **kelele** na mwanafunzi.

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 12, kauli ya utendwa imesababisha yambwa tendewa '*olaiteng'enani*' (mwalimu) kuchukua nafasi ya mtenda. Hivyo basi, baada ya kupachikwa kauli ya utendwa kitenzi elekezi cha yambwa mbili kimebadilika na kuwa kitenzi elekezi cha yambwa moja. Kwa upande mwingine**,** kauli ya utendwa katika uelekezi wa yambwa kapa haisababishi athari yoyote kwa kuwa kitenzi si elekezi hakina uwezo wa kubeba yambwa katika ukomo wake. Hii ni kwa sababu kauli ya utendwa huhusisha mageuzi ya kisintaksia ambayo ni kuhamishwa kwa kipashio yambwa na kukipa hadhi ya mtenda, na mtenda kuhamia sehemu ya yambwa.

### 4.2.5 Athari za Utendewa katika Uelekezi wa Vitenzi vya Kimasai

Athari inayotokea katika uelekezi baada ya mofu ya utendewa kupachikwa katika kitenzi, ni yambwa kuhamia sehemu ya mtenda na kitenzi si elekezi kuwa kitenzi elekezi. Mofu ya kauli ya utendewa ni ***-ak*** na ***-ok***. Hii inadhihirika katika Kimasai kama ifuatavyo;

Kwa upande wa uelekezi wa yambwa moja, kauli ya utendewa haina athari yoyote katika lugha ya Kimasai. Hii inaonekana katika Data Na. 13:

**Data Na. 13:**

Kauli ya utenda
**Kimasai:** *Eiboo engerai **ingishu**.*
**Tafsiri sisisi:** Anachunga mtoto **ng'ombe**.
**Kiswahili:** Mtoto anachunga **ng'ombe**.

Kauli ya utendewa
**Kimasai:** *Eibo-**ok**-ito engerai **ingishu** oo papa.*

**Tafsiri sisisi:** Anachungiwa mtoto **ng'ombe** na baba.
**Kiswahili:** Mtoto anachungiwa **ng'ombe** na baba.

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika kauli ya utendewa hakuna athari yoyote inayotokea katika uelekezi, hivyo kitenzi elekezi cha yambwa moja hubaki kuwa kitenzi elekezi cha yambwa moja, ijapokuwa, kisemantiki mtenda anakuwa mnufaika wa jambo. Kwa upande mwingine, kauli ya utendewa husababisha yambwa tendewa kuhamia sehemu ya mtenda na kufanya kitenzi elekezi cha yambwa mbili kuwa kitenzi elekezi cha yambwa moja. Hii inadhihirika katika Data Na. 14:

**Data Na. 14:**

Kauli ya utenda
**Kimasai:** *Einyang'aka olalashe* ***ilaitengenok olkalamu****.*
**Tafsiri sisisi:** Amemnunulia kaka **mwanafunzi kalamu**.
**Kiswahili:** Kaka amemnunulia **mwanafunzi kalamu**.

Kauli ya utendewa
**Kimasai:** Einyang'-**ak**-aita *ilaitengenok* ***olkalamu*** *oo olalashe**.***
**Tafsiri sisisi:** Amenunuliwa mwanafunzi **kalamu** na kaka.
**Kiswahili:** Mwanafunzi amenunuliwa **kalamu** na kaka.

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 14, athari ambayo imepatikana baada ya kitenzi kupachikwa mofu ya utendewa ni yambwa tendewa kuhamia sehemu ya mtenda, ijapokuwa kisemantiki huyu mtendewa anabaki kuwa mnufaika wa tendo. Kwa upande wa uelekezi wa yambwa kapa**,** athari inayopatikana katika mchakato wa kimofosintaksia wa utendewa ni kitenzi cha yambwa kapa kupokea yambwa ambayo kimuundo inatokea baada ya mtenda. Hivyo, kitenzi kisoelekezi kinabadilika na kuwa kitenzi elekezi cha yambwa moja kama Data Na. 15 inavyoonesha:

**Data Na. 15:**

Kauli ya utenda
**Kimasai:** ***E****tuuror engerai.*
**Tafsiri sisisi:** Ameanguka mtoto.
**Kiswahili:** Mtoto ameanguka.

Kauli ya utendewa
**Kimasai:** *Etuur-**ok**-ine olnjani **engerai*** .
**Tafsiri sisisi:** Ameangukiwa mti **mtoto**.
**Kiswahili:** **Mtoto** ameangukiwa na mti.

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 15, athari inayopatikana hapa ni kuzaliwa kwa yambwa tendwa katika sentensi wakati kitenzi sielekezi kinaponyambuliwa katika kauli ya utendewa. Yambwa hiyo inatokea baada ya mtenda. Hivyo, mofu ya utendewa imesababisha kitenzi kisoelekezi kuwa na uelekezi wa yambwa moja.

### 4.2.6 Athari za Utendeka katika Uelekezi wa Vitenzi vya Kimasai

Katika lugha ya Kimasai, kauli ya utendeka hubadili kitenzi elekezi na kuwa kitenzi si elekezi. Kauli ya utendeka huonyesha hali ya uwezekano wa jambo kufanyika. Mofu ya kauli ya utendeka katika Kimasai ni ***-ai*** na ***-oi***. Hii inadhihirika katika ngazi mbalimbali za uelekezi, yaani uelekezi wa yambwa moja, wa yambwa mbili na wa yambwa kapa.

Katika lugha ya Kimasai, kauli ya utendeka hukiondolea kitenzi sifa ya kuhitaji yambwa katika uelekezi wa yambwa moja . Hii inadhihirika katika Data Na. 16:

**Data Na. 16:**

Kauli ya utendα

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Elepito engoko **kule**.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Anakamua bibi **maziwa**. |
| **Kiswahili:** | Bibi anakamua **maziwa**. |

Kauli ya utendeka

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Elepun-**oi** kule.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Yanakamulika maziwa. |
| **Kiswahili:** | Maziwa yanakamulika. |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Kama inavyooneshwa hapo juu katika Data Na. 16, kauli ya utendeka hubadili kitenzi elekezi cha yambwa moja na kuwa kitenzi si elekezi katika lugha ya Kimasai. Hii ni kutokana na yambwa kuhamia kwenye nafasi ya mtenda, ambaye sasa hahitajiki tena. Pia, kauli ya kutendeka hukiondolea kitenzi sifa ya kuhitaji yambwa katika uelekezi wa yambwa mbili. Hii inadhihirika katika Data Na. 17:

**Data Na. 17:**

Kauli ya utenda

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Eyerakita elatia **ingera endaa*** |
| **Tafsiri sisisi:** | Wanawapikia wanakijiji **watoto chakula**. |
| **Kiswahili:** | Wanakijiji wanawapikia **watoto chakula**. |

Kauli ya utendeka

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Eyer-**ai** endaa.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Kinapikika chakula. |
| **Kiswahili:** | Chakula kinapikika. |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Kama inavyooneshwa hapo juu katika Data Na. 17, kauli ya utendeka imebadili kitenzi elekezi cha yambwa mbili na kuwa kitenzi si elekezi. Hii ni kutokana na yambwa tendwa kuhamia kwenye nafasi ya mtenda, ambaye hahitajiki tena ili kukamilisha taarifa. Hivyo, nomino '*endaa'* (chakula) ni yambwa tendwa inayohama na kuchukua nafasi ya mtenda katika kauli ya utendeka, na nomino '*ingera '*(watoto) ambayo ni yambwa tendewa imedondoshwa. Hata hivyo, data za utafiti huu zinabainisha kuwa kauli ya utendeka haisababishi athari yoyote katika uelekezi wa yambwa kapa. Ili mofu ya kauli ya utendeka ***-ai*** iwe na athari katika uelekezi wa kitenzi ni lazima kitenzi hicho kiwe na uelekezi wa yambwa moja au mbili.

### 3.2.7 Athari za Utendesha katika Uelekezi wa Kitenzi cha Kimasai

Katika lugha ya Kimasai, athari ya kauli ya utendesha ni kuongezeka kwa yambwa yaani kuongezeka kwa mtendwa au mtendewa wa jambo katika sentensi. Kauli ya utendesha hutokana na kumfanya mtu atende jambo fulani. Katika lugha ya Kimasai mofu ya kauli ya utendesha ni ***into, inta*** na ***-ie***. Katika kauli ya utendesha kwa upande wa uelekezi wa yambwa moja, athari inayopatikana ni kuongezeka kwa yambwa moja. Hii inadhihirika katika Data Na. 18:

**Data Na. 18:**

Kauli ya utenda

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Eitooko yeyo **kule.*** |
| **Tafsiri sisisi:** | Anakunywa mama **maziwa**. |
| **Kiswahili:** | Mama anakunywa **maziwa**. |

Kauli ya utendesha

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | ***Into**-oko yeyo **engerai kule**.* |
| **Tafsiri sisisi:** | Anamnywesha mama **mtoto maziwa**. |
| **Kiswahili:** | Mama anamnywesha **mtoto maziwa**. |

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Kauli ya utendesha imesababisha kuongezeka kwa yambwa tendewa lakini yambwa tendwa anabaki na sifa yake ya awali ya utendwa. Hivyo, mofu ya utendesha imesababisha kuongezeka kwa yambwa moja; yaani kutoka kitenzi elekezi cha yambwa moja na kuwa kitenzi elekezi cha yambwa mbili. Kwa upande mwingine, kauli ya utendesha haina athari yoyote katika uelekezi wa yambwa mbili kama Data Na. 19 inavyoonesha:

**Data Na. 19:**

Kauli ya utenda

| | |
|---|---|
| **Kimasai:** | *Inasa eletia **ingerai oloongukuuni*** |
| **Tafsiri sisisi:** | Wanawasimulia wanakijiji **watoto hadithi**. |
| **Kiswahili:** | Wanakijiji wanawasimulia **watoto hadithi**. |

*Kauli ya utendesha

**Kimasai:** *Inasaki **-ie** elatia **oloongukuuni**.*
**Tafsiri sisisi:** Wanasimulisha wanakijiji **hadithi**.
**Kiswahili:** Wanakijiji wanasimulisha **hadithi**.
**Chanzo:** Uwandani (2022)

Data Na. 19 inaonesha kuwa mofu ya kauli ya utendesha inapoongezwa kwenye kauli ya utenda haisababishi athari yoyote, kwani kauli ya utendesha inapopachikwa kwenye kauli ya kutenda husababisha kupoteza maana iliyokusudiwa. Kwa upande wa uelekezi wa yambwa kapa, kauli ya utendesha husababisha kitenzi kuhitaji yambwa. Hii inadhihirika katika Data Na. 20:

**Data Na. 20:**

Kauli ya utenda

**Kimasai:** *Eilepa oltoilo.*
**Tafsiri sisisi:** Inapaa sauti.
**Kiswahili:** Sauti inapaa.

Kauli ya utendesha

**Kimasai:** *Eilep-**ie** engerai **oltoilo**.*
**Tafsiri sisisi:** Anapaza mtoto **sauti**.
**Kiswahili:** Mtoto anapaza **sauti.**

**Chanzo:** Uwandani (2022)

Katika Data Na. 20, athari inayotokea ni uelekezi wa yambwa kapa kuhitaji yambwa katika Kimasai. Kauli ya utendesha imesababisha kutokea kwa yambwa tendwa '*oltoilo'* (sauti). Hivyo kitenzi si elekezi kimekuwa kitenzi elekezi cha yambwa moja.

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa unyambulishaji huathiri uelekezi wa vitenzi vya lugha ya Kimasai kama ifuatavyo: husababisha kuongezeka kwa yambwa (mathalani katika kauli ya utendea, utendewa, utendesha), kuhamishwa kwa yambwa (mathalani katika kauli ya utendeka, utendana, utendeana, utendewa na utendwa), na kudondoshwa kwa yambwa hasa mofu ya kauli ya utendeka inapopachikwa kwenye kitenzi elekezi cha yambwa mbili. Hata hivyo, uelekezi wa vitenzi huathiriwa na unyambulishaji kulingana na sarufi ya lugha husika. Hoja hii imethibitishwa na kauli saba za vitenzi vya lugha ya Kimasai kama zilivyobainishwa na Mollel (2021). Rugemalira (1993) pia anasisitiza kuwa athari za vitenzi hivi hutofautiana kutokana na aina za viambishi vilivyopachikwa kwenye mizizi ya vitenzi hivyo.

Katika kauli ya utendea, makala hii imebainisha kuwa athari inayopatikana ni kuongezeka kwa yambwa katika uelekezi wa yambwa kapa na uelekezi wa yambwa moja. Katika uelekezi wa yambwa moja, yambwa tendewa ndiyo inayoongezeka, na katika uelekezi wa yambwa kapa yambwa tendwa ndiyo inayopachikwa. Hata hivyo, katika uelekezi wa yambwa mbili hakuna athari

yoyote inayotokea. Charwi (2017) anaeleza kuwa kauli ya utendea husababisha vitenzi si elekezi kuwa elekezi katika lugha ya Kikuria hali ambayo hutokea pia katika lugha ya Kimasai. Hoja hii pia inashadadiwa na Khamis (2008) katika kuchambua unyambulishaji wa Kitenzi cha Kiswahili. Aidha, kwa mujibu wa Nadharia ya Uhusika (Chomsky, 1981) kauli ya kutendea hulazimisha kitenzi kubeba muathirika wa tendo linalotendwa.

Katika lugha ya Kimasai, kauli ya utendana huleta athari kwani kitenzi elekezi kikipachikwa mofu ya kauli hii, yambwa huhamishwa kwenda sehemu ya mtenda, na hivyo kuwa kitenzi kisoelekezi. Kwa upande mwingine, kauli ya utendana haina athari yoyote katika uelekezi kapa kwa kuwa kitenzi si elekezi hakina yambwa. Hata hivyo, Charwi (2017) anaeleza kuwa kisintaksia, kauli ya utendana huondoa yambwa kutoka kwenye nafasi yake na kuihamishia kwenye kiima na vipashio vyote viwili, yaani yambwa na kiima hupewa dhima mbili kwa wakati mmoja, yaani mtenda na wakati huo huo huwa mtendwa. Hali hii inadhihirika pia katika Kimasai.

Katika lugha ya Kimasai, vitenzi katika kauli ya utendeana vina uwezo wa kuchukua yambwa moja tu; yambwa tendwa. Hali hii husababishwa na kiima kuchukua majukumu mawili; lile la kutenda na kutendewa. Kauli ya utendeana husababisha kuhamishwa kwa yambwa na kufanya kazi ya mtenda katika uelekezi wa yambwa mbili. Lakini kauli hii inapowekwa kwenye kitenzi elekezi cha yambwa moja na kitenzi si elekezi haisababishi athari yoyote katika sentensi. Hivyo, hufanya kitenzi elekezi kubaki kuwa elekezi cha yambwa moja na kitenzi si elekezi kubaki kuwa si elekezi katika Kimasai.

Katika kauli ya utendwa, Khamis (2008) anasema kiima na yambwa hubadilishana nafasi katika sentensi zalika. Sentensi msingi huwa na kiima ambacho ndicho ‘mtendaji’. Katika kauli ya kutendwa, kiima hicho hupoteza hadhi hii na umuhimu wa kimawasiliano ukawekwa katika kitenzi. Kitenzi katika kauli ya kutendwa huwa na uwezo wa kuchukua yambwa moja tu ambayo ni yambwa tendwa. Hivyo, hata katika lugha ya Kimasai athari hii hutokea ambapo baada ya kupachikwa mofu ya kauli ya kutendwa katika kitenzi cha uelekezi wa yambwa moja na uelekezi wa yambwa mbili husababisha mtenda kuhamia kwenye nafasi ya yambwa, na mtendwa kuchukua nafasi ya mtenda.

Katika lugha ya Kimasai, kauli ya utendewa ni geuzia ya kauli ya utendea ambapo kiima na yambwa hubadilishana nafasi za kisintaksia. Fauka ya hayo, yambwa katika sentensi ya kauli ya utendewa hupoteza umuhimu wa nafasi ya ‘mtenda’ na kuwa kiungo mbadala cha sentensi. Athari inayotokea kati ya uelekezi na kauli ya utendewa husababisha mtenda kuhamia kwenye nafasi ya yambwa katika uelekezi wa yambwa mbili, pamoja na kuongezeka kwa yambwa tendwa katika kitenzi si elekezi. Aidha, mtendaji huwa ni kipashio kisichokuwa cha lazima katika sentensi, maadamu tendo na yambwa tendewa ndivyo vipashio vinavyotiliwa mkazo. Nadharia ya Uhusika inasisitiza pia kuwa kauli ya utendewa husababisha kitenzi si elekezi kuwa elekezi.

Kwa upande wa kauli ya utendeka, katika lugha ya Kimasai kauli hii hukiondolea kitenzi sifa ya kuhitaji mtenda ambaye kisarufi ni mtendaji wa jambo na nafasi hii huchukuliwa na yambwa. Athari ya kauli ya kutendeka hubadili kitenzi elekezi na kuwa sielekezi. Hii ni kutokana na yambwa kuhamia kwenye nafasi ya mtenda, ambaye hahitajiki tena. Hii ni athari ya kisintaksia kwa kuwa inapunguza kipashio kimoja kilichokuwapo awali na kukifanya kisihitajike tena. Khamis (2008) ameonesha kuwa vitenzi vyote vyenye uelekezi vinachukua unyambulishaji punguzi na kuibukia kuwa na sulubu dhima zisizoelekezi.

Aidha, kauli ya utendesha husababisha kuongezeka kwa yambwa, yaani kuongezeka kwa mtendwa au mtendewa wa jambo katika lugha ya Kimasai. Hivyo, kupachika mofu ya kauli ya utendesha kunasababisha kuongezeka kwa yambwa moja katika kitenzi elekezi mara moja na kitenzi sielekezi. Hata hivyo, Khamis (2008) anasisitiza kuwa unyambulishaji ongezaji pia huhusu vitenzi vilivyo katika sulubu dhima zisizoelekezi kuingia katika sulubu dhima za vitenzi elekezi. Hivyo, kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu, matokeo ya makala hii yanaonesha wazi kuwa katika lugha ya Kimasai unyambulishaji unaweza kuathiri kitenzi sielekezi kuwa elekezi kwa kukiongezea, kupunguza au kudhibiti idadi ya vihusika vinavyoambatana nacho.

**4.0 Hitimisho**

Makala hii imechunguza unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa vitenzi katika lugha ya Kimasai. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa lugha ya Kimasai ina aina tatu za uelekezi kama ilivyo katika lugha nyingi, lugha za Kibantu zikijumuishwa. Aina hizo za uelekezi katika Kimasai ni uelekezi wa yambwa moja, wa yambwa mbili na wa yambwa kapa. Hata hivyo, makala hii imebaini kuwa kuna tofauti ya utokeaji wa uelekezi katika lugha ya Kimasai. Katika uelekezi wa yambwa moja, yambwa hujitokeza mara tu baada ya mtenda. Hii ni tofauti na lugha za Kibantu ambapo yambwa hutokea baada ya kitenzi. Kwa upande wa uelekezi wa yambwa mbili, nomino ya yambwa hutokea baada ya mtenda ambapo yambwa tendewa huanza kisha hufuatiwa na yambwa tendwa. Hii pia imekuwa tofauti na lugha nyigine, lugha za Kibantu zikijumuishwa. Hali hii imeibua umuhimu wa utafiti huu kwani ni dhahiri kuwa katika lugha nyingi za Kibantu ambazo tafiti za uelekezi zimefanyika, imeonekana kuwa yambwa hutokea mara tu baada ya kitenzi. Hivyo, utokeaji wa yambwa tendwa na tendewa uliobainishwa na makala hii una mchango katika tafiti tangulizi zinazohusu uelekezi. Pia, makala hii imebaini namna unyambulishaji unavyoathiri uelekezi wa yambwa moja, wa yambwa mbili na wa yambwa kapa. Athari hizo ni kama zifuatavyo: kusababisha kuongezeka kwa yambwa katika kauli ya utendea, kutendewa na utendesha, kuhamishwa kwa yambwa katika kauli ya utendeka, utendana, utendeana, utendewa na utendwa, na kudondoshwa kwa yambwa katika kauli ya utendeka. Kwa kuwa makala hii imejikita katika kipengele kimoja tu cha kiisimu, inapendekezwa kuwa utafiti linganishi unaweza kufanywa katika vipengele

vingine vya kiisimu ili kubainisha mahusiano yaliyopo kati ya lugha za Kinailotiki na lugha nyingine kama zile za Kibantu.

## Marejeleo


Asiimwe, C. (2011). *Unyambulishaji wa Vitenzi katika Lugha ya Runyankole*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Charwi, Z.M. (2017). "Unyambulishaji na Dhana ya Uelekezi katika Lugha ya Kikuria". *Kioo cha Lugha.* 11: 58-77.

Chisia, M. (2012). *Uchanganuzi wa Kauli katika Sentensi Elekezi ya Kiswahili Sanifu*: *Mtazamo wa Nadharia ya Ubanifu*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Chomsky, N. (1981). *Lectures on Government and Binding*. Dordrecht: Foris.

Gitonga, J. (2014). *Upatanishi katika Sentensi ya Kichuka*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Chuka.

Gituru, W.M. (2019). *Unyambulishaji wa Vitenzi katika Kigĩchũgũ*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Chuka.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Haji, M.N. (2018). *Muundo wa Kirai Kitenzi katika Lahaja ya Kitumbatu*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Heine, B. na Nurse, D. (2008). *A Linguistic Geography of Africa*. New York: Cambrige University Press.

Khamis, A.M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mollel, E.S. (2021). *Unyambulishaji wa Vitenzi katika Lugha ya Kimasai-Irkisongo*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Nchimbi, F. (2020). *Utokeaji wa Yambwa na Dhima zake katika Kimatengo na Kiswahili*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Oichoe, M.P. (2005). *Ulinganishi wa Kirai Tenzi cha Kiswahili na Ekegusii Kimofosintaksia: Mtazamo wa Uminimalisti*.Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Rugemalira, J.M. (1993). *Runyambo Verb Extensions and Constraints on Predicate Structure*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha California.

Rugemalira, J.M. (2005). *A Grammar of Runyambo*. Dar es Salaam: LOT Publications.